

LBE 2009 – Migration

Episode 3: Living without documents

Author: Marta Barroso

Editor: Thomas Mösch

Characters:

Narrator 1: female

Narrator 2: male

Inserts (English): male, (42)

Voice (“Passport, please!”, “No passport?”, “No passport!”)

Intro:

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji. Katika kipindi hiki tutakueleza kisa cha mwanamume mmoja kutoka Liberia ameishi maisha ya kujificha. Ameishi humu nchini Ujerumani kwa miaka minne sasa. Ijapokuwa amefaulu kufika alikotaka kwenda, lakini mpaka sasa hana uhakika kama uamuzi aliofanya ulikuwa sawa. Tutaona jinsi anavyoishi na wewe msikilizaji utapata kujuza zaidi juu ya safari yake kutoka Afrika kuja Ulaya. Kwa sababu hana kibali kinachomruhusu kuishi hapa

Ujerumani hatuwezi kulitaja jina lake sahihi katika kipindi hiki. Kwa hivyo tutamwita “John”.

1. SFX: Mixed sounds of journey (lorry, motor boat, sea waves, car)

2. Sound Clip John:

“Ukianza safari kama hii, hufikirii kurudi nyuma. Unafikiria kwenda mbele tu. Hakuna kusimama.”

3. Narrator 1:

John hakufikiria kuwa safari yake hii itamfanya aishi maisha ya kuwa mhamiaji haramu. —maisha ya kuishi chini kwa chini yaani maisha ya kujifichaficha. Kabla hajaanza safari yake, hakufikiria kama siku moja atajikuta kwenye hali kama aliyonayo sasa.

4. Sound Clip John:

“Ukiona kwenye Televisheni, utadhani kwamba Ulaya ni mahala ambapo mtu anaweza kuwa na maisha mazuri.. ni mahala bora, kwenye raha na mafanikio matupu... loo! nimejionea mwenyewe!”

5. Narrator 2:

Nyumbani, Liberia: John ni mkulima, maisha ni mazuri. Lakini anafikiria kuwa kuna uwezekano wa maisha kuwa mazuri zaidi. Na kufanikisha hilo, anaanza safari ya kilomita 5,300 ambayo inamlazimu kuvuka mipaka saba. Safari yake inamchukua miaka minne. Katika kila nchi anafanya kazi ili kupata fedha za kumwezesha kuendelea na safari yake.

6. SFX: Mixed sounds of journey (lorry, barrier opening, sea waves, car)**7. Narrator 1:**

Sasa John ametambua kuwa hajafanikisha kile alichooahidiwa na Televisheni. Anaishi na rafiki yake. Anasafisha nyumba na rafiki yake analipa kodi. John anapika lakini hawezi kununua chakula hana fedha hata za kujinunulia viatu na nguo. Kanisa la Kiprotestanti ndio linamsaidia kumpatia chakula na nguo.

8. SFX: War sounds, shootings**9. Narrator 2:**

Liberia katika mwaka wa 1990 – nchi iliyokumbwa na vita: John anaacha kila kitu na anakwenda kuishi kwenye kambi ya wakimbizi ilio mpakani baina ya nchi yake na Guinea-Conakry. Wakati huu wazo la kutaka kuwa na maisha bora halimtoki akilini. Anapata visa ya kuingia Senegal na hapo anajiunga na watu wengine ambao wana malengo kama yake: Kuondoka Guinea. Hapa ndipo safari yake ilipoanzia.

Sound Clip John:

“Tulipata habari kuwa kuna maajenti, unajua hawa watu wanaohusika na usafirishaji, au uende kwenye uwanja wa magari yanayofanya safari, utawakuta watu wengine huko. Useme tu kuwa unataka kusafiri. Nina nauli na nitasafiri kwa usafiri wa kawadia hadi mahala hapa.”

10. SFX: Mixed sounds of journey (lorry, sea waves, car)

11. Sound Clip John:

“Mwisho wa safari yangu ulikuwa hapa. Hapa kwenye nchi hii, hapa nilipo sasa: Ujerumani. Sasa niko hapa. Swali jingine ni: Itakuwaje? Ninajuliza kila saa, kama kweli ninataka.”

12. SFX: People on the street**13. Narrator 1:**

Hapa Ujerumani, anajaribu kujumuika na jamii. Lakini haiwezekani. Anahofia kuingia mikononi kwa maofisa wa usalama, hofu hii anayo wakati wote. Akipanda basi au treni anahakikisha kuwa hafanyi kosa lolote litakalomfanya afikishwe mbele ya utawala. Hataki kujulikana.

14. SFX: Mixed sounds of journey (car, sea waves, lorry)**15. Sound Clip John:**

“Unapitia kwenye jangwa la Sahara. Hiyo ni safari ya hatari, unajua, kwa sababu ya joto, vumbi na kila kitu. Lazima uwe umejitayarisha kwa hali yoyote ile itakayokukuta.”

16. SFX: Lorry on gravel ground, then fade under**17. Narrator 2:**

Usafiri huo mara nyingi huwa ni wa Lori, Lori aina ya Mercedes 911, ambalo limebadilishwa na kuwa gari la kubeba abiria.

18. Sound Clip John:

“Siwezi kusema ni usafiri wa kawaida kwa sababu huwa limebeba wahamiaji haramu (laughs) (...) “Hakuna mtu aliyekuwa na makaratasi halali.”

19. SFX: Lorry on gravel ground

20. Sound Clip John:

“Huwa tunawaita “pushers”. Kwa sababu wanatakikana walete taarifa, mara nyingine inabidi wapate makaratasi ya uongo ili tuweze kupita.”

21. Voice: “Passport please!”

22. SFX: coins falling, barrier opening, car going away

(fade under)

23. Narrator 2:

Dola 40 – hiki ndicho kiwango anachohitaji kuweza kufika Morocco. Pesa hizi ni baadhi ya fedha alizokusanya na kuweka wakati alipokuwa anafanya kazi ya kulima nchini Liberia. Lakini kiasi kikubwa cha fedha hizo hakitumiki kwa ajili ya usafiri...

24. Sound Clip John:

“Inabidi kuwahonga walinzi wa mipakani. Mpaka tutoe rushwa, pesa, pesa ni mpaka tuwahonge hawa askari wa mpakani, unajua ndio tupate kuvuka. Wenye malori na madereva wanajuana na hawa askari wa mpakani vizuri. Kwa hivyo wanawahonga halafu tunapita.”

25. SFX: Mixed sounds of journey (lorry, sea waves)

26. Sound Clip John:

“Makaratasi yangu yote niliyo kuwa nayo, nilipokuwa Morocco, sasa sina hata moja. Kwa sababu yote yametupwa. Nilipokuwa Uhispania sikutakikana kuwa na karatasi yoyote kwa sababu yangepatikana ningerudishwa Morocco. Na huko ningekamatwa.”

Narrator 1:

Kuna watu ambao wanawaita watu walio kwenye hali kama ya John kuwa ni watu wanaoishi kinyume cha sheria. Lakini sio hivyo ni kwa sababu hawana vitambulisho vyenye kuwatambulisha majina, miaka, mahala alipozaliwa mtu huyo au uraia wake.

27. Voice: “Passport, please!”**28. SFX: heart beating****29. Sound Clip John:**

“Nina hofu kwa sababu ninaishi kinyume cha sheria hapa. Ninaogopa kuulizwa vitambulisho. Ninajitenga sana na shughuli zinazowahusisha watu wengi. Moyo wangu unadunda, yeah. Uso wangu hauonyeshi. Hawawezi kuniona jinsi moyo wangu ulivyo ndani... ninapita bila wasiwasi...kwa sababu ukionyesha wasiwasi usoni....wakikushuku tu basi watataka ujitalbulishe.”

30. Narrator 1:

Mambo mengi yanayotokea kwenye maisha yake kwa sasa yamemkuta bila ya ye ye kutarajia. Japokuwa alikuwa na hamu

kubwa ya kuja Ujerumani, lakini hakujua mengi kuhusu nchi hii, hata ingawa alipewa ushauri kabla ya kuanza safari yake:

Sound Clip John:

“Kwanza utahitajika kutafuta mwanamke, umuowe ili upate kuishi kwenye nchi hiyo. Utapata makaratasi na hivyo ndivyo utakavyo fanikiwa kupata makaratasi mengine, utapata kila kitu bure, kazi na hata nyumba ya kuishi.”

31. SFX: Mixed sounds of journey (car, sea waves, lorry)

Fade under

32. Narrator 2:

Ni safari ya siku mbili kutoka Senegal mpaka Morocco. Anabeba maji mengi na vitafunio vya Kiafrika, mikate, mfuko wenyewe nguo na mswaki. Huo ndio ulikuwa mzigo wake.

33. SFX: Lorry on gravel ground - *Fade under*

34. Sound Clip John:

“Tulikuwa tunazungumza sisi wenyewe kwa wenyewe, tuliulizana kuhusu kile kitakachotupata. Kuhusu ndoto ulizonazo. Kile utakachofanya Ulaya. Mazungumzo kama hayo. (...) kwa mfano vile utakavyo weza kuendelea na safari kutoka Morocco, baada ya kufika hapa utafanya nini. Utaishi vipi.”

35. SFX: Lorry on gravel ground, then fade out

36. Sound Clip John:

“Nilifikiria kuwa mambo yatakuwa mazuri, shwari na kila kitu kitakwenda vizuri kabisa. Nilidhani kuwa nikifika hapa nitapata kazi kwa urahisi, nitapata kibali cha kuishi. Halafu maramoja nianze maisha mapya. Sio kama ilivyo hivi sasa.”

37. SFX: Mixed sounds of journey (lorry, sea waves, car)**38. Narrator 1:**

Bila kibali cha kuishi hapa, hakuna njia nyingine ila kuishi chini kwa chini tu. Kwa mujibu wa sheria yeye hayupo hapa Ujerumani, hatambuliki kwa mujibu sheria za nchi.

39. Sound Clip John:

“Sina marafiki wengi hapa kwa sababu ya hali yangu hii...ninaweza kujiingiza kwenye matatizo. Sina marafiki wengi.”

40. Narrator 1:

Mara nyingine yeye hutembelea mkahawa wa internet. Huko anakutana na marafiki zake wachache. Anasoma, anapika na mara nyingine anabahatika kupata kibarua cha kutengeneza bustani au kusafisha kwa siku moja au mbili. Bila shaka hiyo ni kazi isiyo halali. Yaani anafanya kazi bila serikali kufahamu kwa hivyo anakwepa kulipa kodi.

41. SFX: street traders, then fade under

42. Narrator 2:

Rabat: John anajikimu kimaisha kwa biashara ya kuuza nyembe, krimu za kunyolea na vifaa vya kunyolea. Baada ya miezi minane, amefanikiwa kukusanya dola 1,600. Nusu ya fedha hizo atazitumia kwa safari ya kuvuka bahari ya Mediterranean. Tena sio kwa kutumia feri ya kawaida...

43. SFX: Motor boat, sea waves, then fade under

44. Sound Clip John:

“Hiyo ni sawa na kujinyonga(laughs). Unaweza kurudishwa mara moja. Maanake huna makaratasi. (...) Unakutana nao, unajua biashara wanayoifanya. Wanakuita halafu mnakubaliana, lini utakuwa tayari, saa ngapi, unajua. Unalipa halafu basi hapo unakuwa tayari kwa safari. Tulikuwa kama watu 14 hivi na hao “pushers” wawili – jumla tulikuwa kama watu 16 hivi.”

45. SFX: Sea waves, then fade under

46. Sound Clip John:

“Tulisafiri baharini usiku, sikumbuki tulisafiri kwa saa ngapi. (...) sikuwa na hamu ya kujua, kwa sababu wakati wote nilikuwa nimefumba macho yangu. Naomba tu. Unajua!. Kwa sababu sio wote waliofaulu kukamilisha safari. Huwezi kuamini maji.”

47. SFX: Sea waves, then fade out

48. Narrator 2:

Wakati wa safari hiyo ya kuvuka bahari ya Mediterranean, kama anavyokumbuka, askari walinzi wa pwani ya Uhispania walifika na kumuokoa yeye pamoja na wenzake wengine waliokuwa ndani ya mashua ile. Walipelekwa nchi kavu na kuwekwa wote ndani ya nyumba moja ambako walifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na kuhojiwa.

49. SFX: typing machine (*fade in*)

50. Voice: “No passport?”

53b. SFX: Footsteps running away, then fade under

51. Narrator 2:

Hakuna askari, Kwa hivyo John anakaa hapo kwa siku tano halafu anatoroka. Kwa mara ya kwanza maishani mwake anaanza maisha ya barabarani yaani maisha bila makaazi maalum, lakini ni hapa katika mji wa Marbella, nchini Uhispania ambako anaishi kwa mwaka mmoja kukusanya fedha zitakazo mwezesha kumaliza mkondo wa mwisho wa safari yake.

52. Sound Clip John:

“Nilifanya kazi shambani. Kwenye shamba la nyanya, na pia kwenye shamba la zucchini . Ilinibidi nitumie makaratasi ya mtu

mwingine kuweza kupata kazi nzuri. (...) Ili kujaribu kukusanya fedha za kunifikisha Ujerumani."

53. SFX: Car on street, then fade under

54. Narrator 2:

Sehemu ya mwisho ya safari yake ilimgharimu Euro 280. Rafiki wa rafiki yake ndie aliyemfikisha kwa gari hadi katika mji wa Freiburg, nchini Ujerumani.

55. SFX: Car on street, then fade under

56. Narrator 2:

Hatimae John amefika Bonn, magharibi mwa Ujerumani. Rafiki yake anaeishi hapa na aliyekuwa anategemea kumuona hapa Ujerumani tangu alipoanza safari yake, hayupo amesafiri, ameondoka nchini wiki mbili kabla yeye kufika. Bila anuani nyingine yoyote na kutokujua lugha ya Kijerumani, bila kazi au mahala pa kuishi na bila mke, mwisho wa safari yake umekuwa maisha ya kujificha.

57. Sound Clip John:

"Miaka hii yote niliyoishi hapa, sijawa na maisha halisi. Sijapata mafanikio yoyote tangu nilipofika hapa."

58. SFX: Mixed sounds of journey (lorry, sea waves, car)

59. **Voice:** “No passport!”

60.

Outro:

Na mpaka hapo ndio tumekamilisha makala ya leo katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako, kuhusu uhamiaji. Hadithi hii imeandikwa na Marta Barroso.

Iwapo ungetaka kujua zaidi kuhusu maswala ya uhamiaji ya Ujerumani, tembelea mtandao wa idara kuu ya Uhamiaji na maswala ya wakimbizi: anuani yao ni: w w w . b a m f . d e

Na ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kipingine chochote cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako jiunge nasi kwenye mtandao wetu, anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe Baki salama, Kwaheri!